

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA

05 JUNI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA TAREHE 05 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**530. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Watu wasio na Ulemavu kujiunga na Vyuo vya Watu wenye Ulemavu.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**531. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA
(NEWALA VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Wodi ya Wazazi katika Kituo cha Afya cha Mkwedu - Newala.

532. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaangalia upya mipaka ya Tarafa ya Makambako ambapo Kata 12 zipo Jimbo la Makambako na Kata 5 zipo Jimbo la Lupembe.

533. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa uzio katika Shule ya Sekondari ya Igunga.

534. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga mifereji mikubwa ili kudhibiti mafuriko - Tabora Mjini.

WIZARA YA NISHATI:

**535. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA
(BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme katika Mji wa Biharamulo kwa kukamilisha *Substation* ya Nyakanazi.

WIZARA YA UCHUKUZI:

**536. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Bandari kavu Nang'omba Wilayani Nanyumbu ili kuhudumia mizigo ya Nchi ya Msumbiji.

WIZARA YA KILIMO:

**537. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU
(GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa Mpunga Bonde la Ibanda na kiasi gani kinahitajika kuweka Skimu ya umwagiliaji.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

538. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kukomesha kabisa ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya Watu wengi.

WIZARA YA AFYA:

539. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, mwenendo wa utoaji wa Elimu ya Lishe nchini ukoje.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

540. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya katika Mji Mdogo wa Matai Wilayani Kalambo.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

541. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, kwa kiasi gani ushirikiano kati ya TBS na ZBS unaleta matokeo chanya na kutatua changamoto za Wajasiriamali hususani kutoka Zanzibar.

**DODOMA
05 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**